# TATIZO SI RASILIMALI ZILIZOPOTEA



## Tatizo ni Rasilimaliwatu Tunaowapoteza

Godius Rweyongeza

## Vitabu Vingine Vya Mwandishi Huyu

Songambele sio mgeni kwenye ulimwengu wa uandishi, vitabu vyake ambavyo vimesaidia watu wengi ni pamoja na

1. Kutoka Sifuri Mpaka Kileleni
2. Tatizo Si Rasilimali Zilizopotea (Toleo La Kwanza Na La Pili)
3. Nyuma Ya Ushindi.
4. Mambo 55 Ya Kuzingatia Kabla Ya Kuanzisha Biashara.
5. Jinsi Ya Kuibua Ubunifu Ulio Ndani Yako.
6. Kama Unataka Kuwa Tajiri.
7. Barua Ya Wazi Kwa Wazazi Na Walezi Wa Watoto.
8. Makosa Kumi (10) Wanayofanya Wakulima Na Jinsi Ya Kuyaepuka Ili Kutengeneza Fedha Zaidi.
9. Maajabu Ya Kusoma Vitabu (toleo lililoboreshwa zaidi)
10. Maajabu Ya Kuweka Akiba
11. Tofauti 101 Kati Ya Matajiri Na Masikini
12. Maajabu Ya Kuwekeza Kwenye Hisa, Akiba Na Hatifungani
13. Hatua Kwa Hatua

# TATIZO SI RASILIMALI ZILIZOPOTEA

## Tatizo Ni Rasilimaliwatu Tunaowapoteza

GODIUS RWEYONGEZA (Songambele)

**Jinsi Ya Kusimamia Ndoto Zako Mpaka Zikatimia**

©GODIUS RWEYOGEZA

Disemba 2017
MOROGORO TANZANIA

Haki zote zimehifadhiwa
Hakuna sehemu yoyote ile ya kitabu inaruhusiwa kutolewa upya, kunakiliwa au kuhamishwa kwa namna yoyote ile. Iwe ni kwa njia zinazofahamika sasa hivi au zitakazogunduliwa hapo baadaye bila idhini ya mwandishi.

Mawasiliano: Godius Rweyongeza

Barua pepe: songambele.smba@gmail.com
Tovuti: www.songambeleblog.blogspot.com
YouTube: Godius Rweyongeza
Facebook: @godiusrweyongeza
Instagram: godius_rweyongeza
Simu +255 755 848 391

Maalumu Kwa Watu Wote Wanaotaka Kufanya Mabadiliko Ya Maisha Yao Barani Afrika

# YALIYOMO

Vitabu Vingine Vya Mwandishi Huyu ..................................2

TATIZO SI RASILIMALI ZILIZOPOTEA........................................3

Tatizo Ni Rasilimaliwatu Tunaowapoteza ...............................3

GODIUS RWEYONGEZA..........................................................3

UTANGULIZI ..........................................................................7

DIBAJI ...................................................................................12

Sura ya Kwanza ....................................................................16

TATIZO SI RASILIMALI ZILIZOPOTEA......................................16

Sura Ya Pili ...........................................................................27

TATIZO HUTAKI KULIPA GHARAMA .......................................27

Sura Ya Tatu .........................................................................34

TATIZO UNA HARAKA SANA...................................................34

Sura Ya Nne ..........................................................................44

TATIZO HAUPO TAYARI KUSHINDWA. ...................................44

Sura Ya Tano .........................................................................53

TATIZO NI TABIA. ..................................................................53

Sura ya sita ...........................................................................59

TATIZO HAUNA MALENGO ....................................................59

Sura ya Saba..........................................................................69

TATIZO HUTAKI KUCHOKOZA NYUKI....................................69

Sura Ya Nane....................................................................71

TATIZO NI MARAFIKI WALIOKUZUNGUKA...........................71

Sura ya Tisa......................................................................76

TATIZO NI NIDHAMU .........................................................76

Sura ya Kumi.....................................................................82

TATIZO UNAOGOPA KUCHUKUA HATUA..............................82

Sura ya Kumi na Moja........................................................86

TATIZO NI KUENDELEZA TATIZO BAADA YA TATIZO ............86

Sura Ya Kumi Na Mbili ........................................................97

TATIZO UNARIDHIKA SANA..................................................97

Sura ya Kumi na Tatu.........................................................101

UKIONA VYAELEA...............................................................101

Sura ya Kumi na Nne..........................................................104

TATIZO HUTAKI KUCHEZA MZIKI ULIO NDANI YAKO. .........104

Sura ya Kumi na Tano. .......................................................109

TATIZO HUTAKI KUKUBALI KWAMBA KUNA TATIZO. .........109

Sura ya Kumi na Sita .........................................................113

TATIZO HUTAKI KUFANYA UWEKEZAJI. .............................113

Sura ya Kumi na Saba ........................................................118

TATIZO HUJAFAHAMU MAHALI ULIPO ..............................118

Sura ya Kumi na Nane.......................................................122

TATIZO HUTAKI KUTAFUTA TAARIFA SAHIHI. ....................122

Sura ya Kumi na Tisa. ........................................................126

TATIZO NI UBUNIFU .........................................................126

Sura ya Ishirini ...................................................................129

TATIZO HUJAANGALIA KINACHOENDELEA. .......................129

Sura ya Ishirini na Moja ....................................................133

TATIZO NI KUTOKUWA NA MWISHO .................................133

Sura ya Ishirini na Mbili ....................................................139

TATIZO HUTAKI KUZIONA FURSA.......................................139

Sura ya Ishirini naTatu .......................................................147

TATIZO HUTAKI KUFANYA MAZOEZI ..................................147

Sura ya Ishirini na Nne .......................................................152

Tatizo Unajihurumia Sana..................................................152

Sura ya Ishirini na  Tano ....................................................155

TATIZO HUTAKI KUJITOFAUTISHA MWENYEWE ................155

Sura ya Ishirini Na Sita .......................................................157

Tatizo Hutaki Kusema Hapana ............................................157

Sura ya Ishirini na Saba. .....................................................160

Tatizo Ni Jinsi Unavyoainza Siku Yako. ...............................160

Sura ya Ishirini na Nane. ....................................................165

TATIZO UNATAKA KUFUNGA GOLI LA MKONO .................165

Sura ya Ishirini na Tisa .......................................................167

TATIZO UNAOGOPA. ....................................................................167
Sura ya Thelahini ........................................................................173
TATIZO HUTAKI KUPANGILIA VITU VYAKO...........................173
Sura ya Thelathini na Moja ............................................................183
TATIZO NI MATUMIZI YA MUDA....................................................183
Sura ya Thelathini na Mbili ............................................................187
TATIZO UNASUBIRI MPAKA UTAKAPOKUWA TAYARI.........187
Sura ya Thelathini na Tatu ............................................................190
TATIZO HUFANYI KAZI KWA WAKATI SAHIHI. ....................190
Sura Ya Thelathini Na Nne ............................................................192
TATIZO HUTAKI KUANZA.........................................................192
Sura ya Thelathini na Tano ............................................................194
TATIZO HUJAZIJUA KANUNI HIZI...............................................194
Sura ya Thelathini na Sita ............................................................196
TATIZO NI KAULI MBIU HIZI ULIZO NAZO ..........................196
Sura Ya Thelathini Na Nane ............................................................209
Tatizo Hujajua Kwamba Pesa Ni Wazo ..............................209
Sura Ya Thelathini na Tisa ............................................................218
TATIZO NI KAULI ULIZOAMBIWA ...........................................218
Sura ya Arobaini..........................................................................222
TATIZO  HUTAKI KUWEKA AKIBA. .......................................222
Sura ya Arobaini Moja ...................................................................226

TATIZO UMEENDEKEZA UTUMWA HUU ............................226
Sura Ya Arobaini Na Mbili ..................................................229
TATIZO UMEPEWA MAANA MBAYA NA UMEIKUBALI........229
Sura ya Arobaini na Tatu....................................................233
TATIZO UNAWEKA BAJETI SEHEMU ISIYOTAKIWA ............233
Sura Ya Arobaini na Nne ...................................................236
TATIZO HUTAKI KUONGEZA THAMANI ...............................236
Sura Ya Arobaini na Tano..................................................241
TATIZO UNALALAMIKA SANA ............................................241
Sura ya Arobaini na Sita ....................................................244
TATIZO HUJAJUA MAMBO AMBAYO YATAKUPELEKEA USHINDI ..........................................................................244
Sura ya Arobaini na Saba ...................................................249
TATIZO UNAONA UBAYA KATIKA UZURI ............................249
Sura ya Arobaini na Nane ..................................................251
TATIZO HUTAKI KUTOA KAULI HII ......................................251
Sura ya Arobaini na Tisa ...................................................252
TATIZO NI RASILIMALI WATU TUNAZOZIPOTEZA. ..............252
Sura Ya Hamsini ................................................................264
TATIZO HUJAJUA KWAMBA MAISHA NI MCHEZO .............264
Sura Ya Hamsini na Moja ...................................................270
TATIZO HUJAJUA UMUHIMU WA NENO MOJA .................270

Sura Ya Hamsini na Mbili ....................................................272
TATIZO HUTAKI KUJIFUNZA KUTOKA KWENYE MAKOSA YA ZAMANI .........................................................................272
Sura ya Hamsini na Tatu ....................................................274
TATIZO UNAJIDHARAU SANA.............................................274
Sura ya Hamsini na Nne.....................................................279
USIRUKE NGAZI..................................................................279
Sura ya Hamsini na Tano ...................................................284
WASHINDI NI WATU WA SHUKRANI..................................284
Sura ya Hamsini na Nne.....................................................286
IHESHIMU SHERIA YA KUZIDISHA ......................................286
Sura ya Hamsini na Saba....................................................288
MAISHA NDANI YA DARASA NI TOFAUTI NA MAISHA NJE YA DARASA..............................................................................288
Sura ya Hamsini na Nane....................................................291
TATIZO HUTAKI KUKUTANA NA WEWE. ............................291
Sura ya Hamsini Na TISA....................................................293
TATIZO HUWAONI WATU WENGINE .................................293

# UTANGULIZI

Kwa siku nyingi sasa kumekuwepo na malalamishi kutoka kwa watu mbalimbali, ndani na nje ya bara la la AFRIKA, malalamishi haya haswa yanaelekezwa kwa wazungu na wakoloni na watu nchi za nje. Watu wengi wamekuwa wakilalamika kwamba sasa bara la Afrika lingekuwa limepiga hatua kubwa sana kama wasingekuwa wakoloni waliotawala nchi hizi za Afrika na kuchukua rasilimali nyingi sana. Katika kitabu hiki utakutana na mtazamo wa tofauti kutoka kwa mwandishi. Mwandishi atakuonesha kwamba rasilimali zilizopotea si tatizo kama ambavyo watu wengi wanafikiri. Hii ni kutokana na ukweli kwamba rasilimali bado zinazidi kupotea mpaka sasa hivi. Kila mtu ni shuhuda juu ya madini, wanyamapori na mchanga ambao umekuwa ukizidi kubebwa na kupelekwa nje ya nchi kila mwaka, ingawa wakoloni hawapo.

Si hilo tu bali watanzania na waafrika kwa ujumla wamezidi kuwa nyuma kwa mambo mengi ikiwemo mambo ya uwekezaji, uhuru wa kiuchumi, sayansi, utafiti kutaja ila machache.

Hii ni kutokana na imani ya watu wengi ambao wanaamini kwamba mwekezaji ni mtu kutoka nje ya

nchi na wengine wanaamini kwamba vitu vingine si vya viwango vyao bali vinastahili kufanywa na wazungu. Basi kwa hali hii bila shaka utakubaliana na mimi kwamba TATIZO SI RASILIMALI ZILIZOPOTEA.

Sasa kama tatizo si raslimali zilizopotea tatizo ni nini?

Katika kitabu hiki utapata kujifunza kwamba rasilimali watu zinazopotea sasa hivi. Kwa sasa tunazipoteza rasilimaliwatu kwa njia nyingi sana. Hii ni kutokana na watu wengi kutokujua kwamba wanao uwezo mkubwa sana ndani yao ambao wanapaswa kuutumia ili uwatoe sifuri mpaka kileleni. Njia hizo zinazosababisha tupoteze rasilimali watu, sasa zimeelezwa ndani ya kurasa za kiabu hiki.

Vijana sasa wanashinda katika vijiwe vya zama za taarifa ambayo ni mitandao ya kijamii kama *wasapu*, *instagram*, *twitter*, na *facebook*. Vijana wanapoteza muda mwingi kujadili vitu ambavyo havina manufaa kwao na kwa jamii yetu. Vijana wengi wanaamini kwamba mtu fulani ambaye yuko sehemu fulani katika nchi fulani ndiye anayehusika na kufanikiwa kwao. Ndio maana muda mwingi sana unawakuta mtandaoni wakipoteza muda kwa kujadili vitu ambavyo havina maana. Wanalamikia serikali juu ya ajira. Lakini vijana hao hao unawakuta wanazurura mtaa mmoja mpaka mwingine.

Wanazurura kutoka kwa mjomba kwenda kwa shangazi mara kwa bibi, mara kwa babu upande wa mama kizaa mama. Wanazurura kwa kisingizio cha kwamba hawana ajira au kisingizio cha ninatafuta ajira.

Lakini hata hivyo wale wanaowapokea nao wanazidi kusababisha tupoteze rasilimali muhimu ambazo zingeweza kuanzisha kitu. Rasilimali ambazo zimesubiriwa zina mziki ndani yao, rasilimali zenye viwanda katika fikra zao.

Kila mtu kazaliwa akiwa mshindi, na kila mtu ndani yake zimewekwa mbegu za ushindi. Maisha mazuri, utajiri, ushindi, mahusiano mazuri, amani, kazi nzuri na biashara iliyofanikiwa. Vyote hivi ni haki ya kuzaliwa ya kila mtu. Lakini kuzaliwa ukiwa mshindi haitoshi. Kama haupo tayari kulipa gharama ya ushindi. Unapaswa kujua wapo unaenda na kwa nini unaenda huko.

Kila mara jiulize swalije, mimi……(weka jina lako) niko wapi? Ninafanya nini? Je, nimekuja hapa kufanya nini? Kama utajikuta hufanyi kile ambacho unapswa kufanya hata kama wewe umezaliwa mshindi, my friend, ushindi utausikia redioni. Umezaliwa mshindi lakini unapaswa kuhakikisha kwamba unalipa gharama ya ushindi na kufanya kazi kiushindi kila wakati.

Kisome kitabu hiki mwanzo mpaka mwisho maana kuna mambo mengi sana ya kujifunza. Hakika usiruke wala kutafuta sura ambazo wewe unaona kama zinakufaa. Wewe ni mtu wa muhimu sana na jamii nzima imesubiri na inataka kusikia kutoka kwako. Badili mtazamo wako ili uweze kubadili maisha yako.

Kuna uwezo mkubwa sana ndani yako ambao bado haujaufahamu na bado haujaanza kuutumia. Kama wewe ni moja ya watu ambao wangependa kuutumia uwezo huu mkubwa ulio ndani. Kama wewe ni moja ya watu ambao wangependa kuitumia dhahabu hii kubwa sana ambayo haijachomwa hata kidogo, basi kitabu hiki kinakufaa sana, kwa hakika umeshikilia hazina itakayobadili maisha yako. Badili fikra zako kwa kusoma kitabu hiki. Haitoshi tu wewe kusoma kitabu hiki na kutulia. Hatua madhubuti zinapaswa kuchukuliwa baada ya wewe kusoma kitabu hiki. Msimamo wa mwandishi ni ule ya kwamba mtu yeyote anaweza kukuweka katika njia sahihi, lakini hawezi kukuamrisha wewe kuitembea njia hiyo. Kitabu hiki kinaonesha njia tu! Ila suala zima la kuifuata njia hiyo lipo juu yako.

Wewe Ni Zaidi Ya Ulivyo Sasa

Chukua hatua sasa

Tukutane kwenye meza ya wanamafanikio!!!!

Tukutane kwenye mzunguko wa wanamafanikio!!!

Ndimi,

Godius Rweyongeza

($onga mbele)

Kocha, mjasiliamali na mwandishi

# DIBAJI

TATIZO SI RASILIMALI TULIZOZIPOTEZA ni kitabu kilichokuja kwa wakati muafaka. Ni kitabu kilichosheheni hekima ya hali kubwa sana isiyo ya kawaida.

Watu wengi tumekuwa tukiona na kulalamika kwamba rasilimali za nchi zinapotea lakini mwandishi wa kitabu hiki amekuja kwa namna ya tofauti kabisa akisema Tatizo Si Rasilimali Zilizopotea, tatizo ni rasilimali watu tunazozipoteza.

Wakati unaponyoosha kidole kimoja ukilalamikia watu fulani kumbuka vidole vitatu vinaelekea kwako huku kidole gumba kikielekea kwa Mungu kuonesha ushuhuda ya kwamba tatizo ni wewe wala sio mtu mwingine yeyote. Kwa mantiki hiyo mwandishi ametutaka tutumie nguvu tuliyoibeba sisi wenyewe ambayo ndiyo nguvu kubwa kuliko zote. Nguvu hiyo ni akili. Kama kila mtu akiweza kutumia akili yake kwa kiwango kinachotakiwa tunaweza kuona maajabu makubwa katika jamii zetu.

Kila mmoja akijimudu kwa kila eneo alilopo tunategemea mabadiliko katika karne hii ya ishirini na moja.

Katika kitabu hiki pia utapata kujifunza somo muhimu sana ambalo ni PESA. Wakati kama huu ambapo kila unayekutanana naye  analalamika akisema **“VYUMA VIMEKAZA.”** Mwandishi wa kitabu hiki amekuletea grisi ambayo itasaidia kuvilainisha vyuma vilivyokaza, yaani ukiweza kujifunza kuhusu pesa, hautakuwa mtu wa kusema “Vyuma vimekaza.”

Nakubaliana na mwanamuziki B.B. King aliyewahi kusema **“Kitu kizuri kuhusu kujifunza ni kwamba hakuna mtu anayeweza kukupokonya yale uliyojifunza.”** Kumbe kitabu hiki ni cha lazima kukisoma tena watu wa rika zote.

ONYO!! Usikubali kitabu hiki kipite mikononi mwako bila kukisoma.

Pongezi za pekee kwa Mwandishi mashuhuri, Godius Rweyongeza kwa kutulete kitabu hiki cha karne ambacho yeyote atakayekisoma hakika hawezi kujuta. Lazima awe mtu mpya. TATIZO SI RASILIMALI TULIZOZIPOTEZA, TATIZO NI RASILIMALI WATU TUNAZOZIPOTEZA.

Edius Katamugora

Mwandishi kitabu cha BARABARA YA MAFANIKIO.